



## MBALIZI C.D HOSPITAL

## MBALIZI EVANGELISTIC CHURCH

S. L.P 6117

P. O. Box 6117

MBEYA

MBEYA

Simu +255 25 2561004/5/6

Tel. +255 25 2561004/5/6

Fax +255 25 2561006

Fax +255 25 2561006

E-mail: mbalizihospital@gmail.com

**13/12/2019**

## TANGAZO LA KAZI

Hospitali ya Mbalizi ni hospitali teule ya Wilaya ya Mbeya na inamiliwa na Kanisa la Uinjilisti Tanzania iliyo na makao makuu yake katika mji mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya. Hospitali inatangaza nafasi za kazi kada zifuatazo;

### 1. Afisa muuguzi Daraja la II (Nafasi 6)

#### 1.1 Sifa

Awe amehitimu stashahada (diploma)ya uuguzi ya muda usiopungua miaka miwili kutoka chuo kinachotambuliwa na serikali waliosajiliwa na baraza la wauguzi na wakunga Tanzania

#### 1.2 Kazi na Majukumu

- i) Kutoa huduma za uuguzi
- ii) Kukusanya takwimu muhimu za afya
- iii) Kuwaelekeza kazi wauguzi waliochini yake
- iv) Kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu matatizo yao ya kiafya
- v) Kutoa huduma zingine za kinga na uzazi
- vi) Kufanya kazi nyingine atakazo pangiwa na mkuu wake wa kazi

#### 1.3 MSHAHARA

#### 1.4 Utalipwa mshahara wakuanzia na TGHS B

## **2. Muuguzi Daraja la pili (Nafasi 16)**

### **2.1 Sifa**

Awe amehitimu Astashahada Uuguzi ya miaka miwili kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali na kuandikishwa (Enrolled) na Baraza la Wakunga Tanzania.

### **2.2 Kazi na Majukumu**

- i) Kufanya kazi za kiuguzi za kuhudumia wateja katika jamii, hospitali na sehemu zote zinapotolewa huduma za afya
- ii) Kusimamia na kuratibu kazi zote za wahudumu wa afya katika sehemu yake ya kazi
- iii) Kutoa huduma kwa wagonjwa majumbani
- iv) kutoa ushauri na saha
- v) Kusanya takwimu na kutayarisha taarifa za utendaji wake wa kazi
- vi) Kutoa huduma za kinga na uzazi wa mpango
- vii) Kutoa huduma za na afya ya motto
- viii) Kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu matatizo yao ya kiafya
- ix) Kufuatilia utunzaji wa vitendea kazi katika maeneo yake ya kazi
- x) Kufanya kazi nyingine atakazo pangawa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

### **2.3 MSHAHARA**

**Utalipwa mshahara kuanzia na TGHS A**

### **3. Mteknolojia Msaidizi Dawa (Nafasi 1)**

#### **3.1 Sifa**

Awe amehitimu astashahada ya mteknolojia msaidizi wa dawa kwa miaka miwili kutoka chuo kinachotambuliwa na serikali na ambae amesajiliwa.

#### **3.2 Majukumu na kazi**

- i) Kuandaa mahitaji na matumizi ya dawa na vifaa
- ii) Kuagiza, kuhifadhi na kugawa dawa na vifaa tiba katika eneo lake la kazi
- iii) Kuandaa taarifa ya matumizi ya dawa na vifaa tiba
- iv) Kutunza kumbukumbu za dawa na vifaa tiba
- v) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

#### **3.3 MSHAHARA**

Utalipwa mshahara wakuanzia na TGHS A

### **4. Muudumu wa Afya (Nafasi 4)**

#### **4.1 Sifa**

kuajiriwa wahitimu wa kidato cha nne waliopata mafunzo ya mwaka mmoja katika fani ya afya

#### **4.2 Kazi na majukumu**

- i) Kufanya usafi wa vifaa vyatia kazi, usafi wa wodi na mazingira
- ii) Kusaidia wagonjwa wenyewe ulemavu na wasiojiweza katika kwendas haja (kubwa na ndogo) na kuoha
- iii) Kumsaidia kumlisha mganjwa asiyejiweza
- iv) Kuchukua nguo za mganjwa kupeleka kwenda kufuliwa
- v) Kuchukua sampuli za mganjwa kwaajili ya vipimovya maabara na kufuatilia majibu
- vi) Kutayarisha vifaa kwaajili ya kusafisha na kufunga majeraha
- vii) Kufuatilia mahitaji ya dawa kwa wagonjwa kutoka hifadhi ya dawa
- viii) Kufanya shughuli nyingine atakazo pangia na kiongozi wake wa kazi

#### **4.3 MSHAHARA**

Utalipwa mshahara wa kuanzia na TGHOS A

## **5. Namna ya kuomba**

Maombi yote yaambatanishwe na;

- i) Maelezo binafsi (Curriculum vitae)
- ii) Vyeti vilivyo thibitishwa (Certified Certificates)
- A) Cheti cha taaluma pamoja na cheti cha mafunzo kwa vitendo
- B) Lesseni
- C) Cheti cha sekondari (kidato cha iv na kidato cha vi)
- D) Cheti cha kuzaliwa
- E) Kitambulisho cha NIDA/ Namba ya NIDA
- F) Mwombaji awe mtanzania asiye zidi umri wa miaka 45

6. Maombi yote yatumwe kwa;

**MGANGA MFAWIDHI**

**HOSPITALI YA MBALIZI**

**S.L.P 6117**

**MBEYA.**

**Barua pepe:mbalizihospital@gmail.com**

**SIMU 0735542568**

**Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 10/01/2020 saa 9:30 Alasiri**